Sera ya Muundo Mbadala wa Mifumo ya Haki

MIFUMO YA KITAMADUNI, ISIYO RASMI NA MINGINEYO INAYOTUMIKA KUPATA HAKI NCHINI KENYA (MIFUMO MBADALA YA HAKI)

AGOSTI 2020

Shukurani

Shukurani za kipekee kwa Taasisi ya Denmark ya Haki za Binadamu kwa kuwezesha mchakato wa kutafsiri sera ya AJS ili kuboresha uzoefu wa mafunzo kwa kutoa chaguo zaidi za lugha ya sera hii.

THE DANISH
INSTITUTE FOR
HUMAN RIGHTS

1.0 Utangulizi

Hakimiliki © Mahakama ya Kenya, 2020

Imechapishwa na
Mahakama ya Kenya
SLP 30041 - 00100, Nairobi Simu. +254 20 2221221

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoweza kunakiliwa au kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki au kimitambo, ikiwemo kunakili, kurekodi au kwa mfumo wowote wa kuhifadhi na kurejesha taarifa, bila kibali kwa njia ya maandishi kutoka kwa mwandishi au kutambua asili yake isipokuwa kwa kujumuisha nukuu fupi kutoka kwa uhakiki.

Picha ya jalada: Allan Gichigi/UNODC
Kubuni na mpangilio: Amina Darani/UNODC

Funded by the European Union

Chapisho hili lilitolewa kwa usaidizi wa kiufundi kutoka Afisi ya Umoja wa Mataifa wa Dawa na Uhalifu (UNODC) na kwa usaidizi wa kifedha wa Umoja wa Ulaya kupitia Mpango wa Uwezeshaji wa Kisheria na Utoaji Misaada nchini Kenya (PLEAD). Yaliyomo ndani yake ni jukumu la Mahakama ya Kenya na hayaakisi maoni ya Umoja wa Ulaya au UNODC.

Sera ya Muundo Mbadala wa Mifumo ya Haki

MIFUMO YA KITAMADUNI, ISIYO RASMI NA MINGINEYO INAYOTUMIKA KUPATA HAKI NCHINI KENYA (MIFUMO MBADALA YA HAKI)

AGOSTI 2020

Kuoanisha Mbinu za AJS na Mahakama na Katiba ya Kenya (2010) na Mfumo wa Mahakama wa Kudumisha Mabadiliko ya Mahakama

Akronimi na Vifupisho

ADR	Utatuzi Mbadala wa Mizozo
AJS	Mifumo Mbadala ya Haki
CEDAW	Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake
CRA	Tume ya Ugawaji Mapato
CRC	Mkataba wa Haki za Mtoto
CSO	Shirika la Kijamii la Kutetea Masuala ya Raia
CUC	Kamati ya Watumiaji Mahakama
DPP	Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma
GJLOS	Sekta ya Utawala, Haki, Sheria na Utaratibu
ICESCR	Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni
ICCPR	Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa
IEBC	Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka
JSC	Tume ya Huduma ya Mahakama
KNCHR	Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za Binadamu
NGO	Shirika lisilo la Kiserikali
NLC	Tume ya Kitaifa ya Ardhi
NPSC	Tume ya Kitaifa ya Huduma ya Polisi
PSC	Tume ya Huduma ya Umma
SRC	Tume ya Mishahara na Marupurupu
SWOT	Uwezo, Udhaifu, Nafasi, Matishio
UDHR	Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu

Dibaji

Mojawapo ya kanuni za msingi zilizowekwa kwenye Katiba ili kuongoza utoaji wa haki na utekelezaji wa mamlaka ya mahakama, ni hitaji la kukumbatia njia mbadala za utatuzi wa mizozo, ikiwemo mifumo ya jadi ya utatuzi wa mizozo. Shart hili ni badiliko la kimsingi kuanzia mtazamo hadi wazo na dhana ya haki, hasa katika muktadha wetu wa Kenya. Jamii za Kenya, kwa vizazi kadhaa, zimeunda mifumo yao ya haki ambayo imekuwa na inaendelea kushikilia jamii pamoja. Huku haki inayotolewa na Mahakama ikichukua nafasi kuu katika utoaji wa haki, ukweli ni kwamba idadi kubwa ya mizozo (Sera hii inakadiria takriban asilimia 90) miongoni mwa Wakenya inatatuliwa kupitia mifumo ya haki ambayo inatofautiana na mchakato rasmi wa Mahakama. Kwa hivyo, mwongozo wa kikatiba wa kukubali na kutambua Mifumo Mbadala ya Haki unapatikana kwenye mfumo mpana wa mwitikio ambao unashughulikia, kiujumla, dhana ya haki katika muktadha wa Kenya.

Ni katika muktadha huo hapo juu ambapo mtangulizi wangu, Jaji Mkuu Mstaafu Dkt Willy Mutunga aliteua Jopokazi la mifumo ya kitamaduni, isiyo rasmi na mingineyo ya kutatua mizozo nchini Kenya. Jopo hilo lilitakiwa kuchunguza chaguzi za kikatiba, kisheria na kisera zinazopatikana ili kutimiza matakwa kwenye Ibara ya 159 (2) ya Katiba. Muhimu zaidi, Mahakama kupitia miongozo yake muhimu (Mfumo wa Mabadiliko ya Mahakama (2011-2016) na Kudumisha Mabadiliko ya Mahakama 2017-2021) imeweka mikakati, mipango, na sera za kitaasisi ili kuzingatia na kutambua mifumo mbadala ya haki. Hivyo basi, Sera ni matokeo muhimu kwa mustakabali wa utoaji haki, na haswa, jinsi huduma za mahakama zinavyoweza kutolewa huku zikitilia maanani mchakato mpana wa utoaji haki nchini.

Hakuna shaka kwamba Mifumo Mbadala ya Haki ina matumaini makubwa katika kuimarishwa kwa upatikanaji wa haki, katika maana kamili ya dhana hiyo. Sera hiyo inatoa mapendekezo ya wazi na chaguzi zinazowezekana kuhusu jinsi mfumo wa mahakama na Mifumo Mbadala ya Haki inaweza kuingiliana kwa njia ambayo inaimarisha na kulenga mfumo bora wa haki. Sera hiyo pia imebainisha hatua muhimu na za haraka za kuchukuliwa ili kusisimua kipengele hiki muhimu cha utoaji haki. Hatua hizi ni pamoja na: utambuzi wa masuala ya kuletwa chini ya AJS, udhibiti wa wahusika wa AJS, taratibu na michakato inayofaa katika AJS, uingiliaji unaofaa, na ugawaji wa rasilimali ili kusaidia mchakato huo.

Hata hivyo, ni muhimu kwamba Sera hiyo ionekane kama hatua kuu ya kuelekea katika kutimiza ajenda ya Mabadiliko ya Katiba ya Kenya ya 2010. Kupitia kuibua uwezo wa kuleta mageuzi wa Mifumo Mbadala ya Haki na kukumbatia sheria ya kijamii na kihali inayohitajika na Katiba, Sera hiyo inatoa nafasi ya mazungumzo kwa Mahakama na Mifumo Mbadala ya Haki ili kutoa maono ya mabadiliko ya Katiba ya Kenya: kugeuzwa kwa miundo inayosababisha ukandamizaji wa kijinsia; udhalimu wa kijamii na unyanyapaa; utawala wa kitamaduni; dhuluma za ugawaji na za kijamii na aina nyingine za ukandamizaji.

Sera hiyo ni mwongozo muhimu katika uendeshaji wa Mifumo Mbadala ya Haki, sio tu kwa Mahakama, bali kwa taasisi zote za sekta ya haki. Nashukuru jopo zima, chini ya uongozi wa Mhe. Jaji (Prof.) Joel Ngugi, kwa kazi hii muhimu itakayosaidia kufafanua sehemu muhimu katika utoaji haki nchini.

Mhe. Jaji David K. Maraga, EGH

Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Kenya
na Rais wa Mahakama Kuu

Nairobi
Agosti 27, 2020

Yaliyomo

Akronimi na Vifupisho iv

Dibaji v

Muhtasari viii

1.0 Utangulizi 1

1.1. Usuli 1

1.2. Mchakato wa kuunda sera hiyo 1

1.3. Mtazamo wa Kihistoria 2

2.0 Mantiki na Muktadha 3

2.1. Mazingira yaliyopo 3

2.2. Masharti ya Kujihusisha na AJS 3

2.2.1. Matakwa ya Katiba 3

2.2.2. Mifumo ya Kikanda na Kimataifa 3

2.2.3. Umuhimu wa AJS 4

2.2.4. Changamoto kwa Kazi za AJS 5

2.2.5. Uchanganuzi wa SWOT 6

3.0 Mipango ya Sera ya AJS 7

3.1. Mfumo wa Haki za Binadamu na mbinu za AJS 7

3.1.1. Wajibu wa Kuheshimu 7

3.1.2. Wajibu wa Kulinda 7

3.1.3. Wajibu wa Kubadilisha 7

3.2. Miundo ya AJS na Mapendekezo ya Sera 7

3.2.1. Taasisi Huru za AJS 8

3.2.2. Taasisi za AJS zenye Wahusika wa Tatu Zilizo Huru: 8

3.2.3. Taasisi za AJS Zilizounganishwa na Mahakama 8

3.2.4. Taasisi za AJS Zilizodhibitiwa 8

3.3. Mwingiliano kati ya mbinu za AJS na mahakama 8

3.4. Mkakati wa Haki ya Kijamii wa AJS 9

4.0 Maeneo ya Uingiliaji Kati wa Sera ya Kimkakati 10

5.0 Maeneo ya Uingiliaji Kati wa Sera ya Utendakazi 11

5.1. Kubaini na Kutambua Hali ya Kesi ambazo AJS inaweza kusikiliza 11

5.2. Kuimarisha michakato ya uteuzi, uchaguzi na kuondolewa kwa wahusika wa AJS 12

5.3. Kuendeleza taratibu na sheria za Mifumo ya Haki Mbadala 12

5.4. Kuwezesha uingiliaji kati ufaao wa mwamuzi 13

5.5. Ugawaji rasilimali na uhamasishaji ulioimarishwa na endelevu 13

6.0 Masuala Mtambuka 14

7.0 Wahusika, Michakato na Taratibu za Utekelezaji 15

7.1. Wahusika 15

7.2. Utaratibu wa Utekelezaji 15

8.0 Ufuatiliaji na Tathmini 17

9.0 Uhakiki wa Sera 27

Viambatisho 18

Muhtasari

Tarehe 4 Machi 2016 aliyekuwa Jaji Mkuu, Mhe. (Dkt) Willy Mutunga aliteua Jopokazi la Mifumo Mbadala ya Haki kutathmini Mifumo mbalimbali *ya Kitamaduni, Isiyo Rasmi na Mingineyo Inayotumiwa Kupata Haki Nchini Kenya (Mifumo Mbadala ya Haki)* na kubuni sera ya kitaifa kuhusu Upatikanaji wa Haki. Kwa zaidi ya miaka minne, Jopokazi, ambalo muda wake uliongezwa hadi Aprili 2020 na Jaji Mkuu Mhe. David Maraga, lilifanya utafiti, kuenda nyanjani, na mashauriano ya kina na washikadau. Kazi ya Jopokazi hilo ilisababisha kuwepo kwa rasimu ya sera - *Haki kama Uhuru: Mifumo ya Kitamaduni, Isiyo Rasmi na Mingineyo ya Utatuzi wa Mizozo nchini Kenya* - ambayo hutumika kama mpango wa utekelezaji na uingiliaji kati kuanzisha Mifumo Mbadala ya Haki (AJS). Sera hii ya Muundo wa AJS (Sera) ni matokeo ya kazi ya Jopokazi.

Sera hiyo inachukulia AJS kuwa kipengele muhimu cha kupata haki na lengo lake kuu ni kutekeleza Ibara ya 159(2)(c), ambayo inaidhinisha Idara ya Mahakama, kama chombo cha Serikali, ili kukuza AJS. Katika ngazi ya kimataifa, AJS ni mfumo wa kuhakikisha upatikanaji wa haki chini ya Lengo la 16 la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa, ambalo linawajibisha viongozi wake 'kukuza jamii zenye amani na umoja kwa ajili ya maendeleo endelevu, kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye ufanisi, uwajibikaji na shirikishi katika ngazi zote'.

Mamlaka: Mamlaka ya sera ya AJS ni kutimiza matakwa ya Ibara ya 159(2) (c) ya Katiba ya (2010) na uzoefu wa kila siku wa haki wa Wakenya na kwa kufanya hivyo kupendekeza mikakati ya kujumuisha na kudumisha kazi huru za utaratibu wa AJS kwa kutumia mbinu zinazoafiki kizingiti cha Katiba ya Kenya na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

Maono: Uhuru mpana, upatikanaji na matokeo ya haki yenye ushirikishwaji na usawa kwa wote nchini Kenya.

Misheni: Kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa njia ya ufanisi kwa kuheshimu, kulinda na kubadilisha mbinu za AJS nchini Kenya.

Mipango ya Sera

Jopokazi lilitambua maeneo matano ya kimkakati ya kuingilia kati, kila moja ikiwa na shughuli zinazolingana. Hizi ni:

1. Utambuzi rasmi wa Mifumo Mbadala ya Haki na utambuzi wa aina za kesi ambazo AJS inaweza kusikiliza.
2. Kuimarisha mchakato wa uteuzi, uchaguzi na kuondolewa kwa wahusika wa AJS;
3. Maendeleo ya taratibu na sheria za kimila;
4. Uwezeshaji wa uingiliaji kati wenye ufanisi; na
5. Ugawaji na uhamasishaji wa rasilimali ulioimarishwa na endelevu.

Waraka huu wa mfumo unapaswa kusomwa pamoja na waraka mkuu, Sera ya Msingi ya Mifumo Mbadala ya Haki.

1.0 Utangulizi

1.1 Utangulizi

Mifumo Mbadala ya Haki (AJS) ni dhana ya kifalsafa na vile vile desturi ya kupata haki. Kama dhana ya kifalsafa, na inayoendana na shule ya mawazo ya haki za binadamu, imejikita katika mawazo ya kimsingi yafuatayo: uhuru, usawa, kutobaguliwa, utu na usawa. Haya yote yamo katika Katiba ya Kenya. Kama desturi ya kupata haki, AJS inarejelea hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kufikia usawa kwa wanachama wote wa utambulisho fulani wa kitamaduni, kisiasa na kijamii. Kwa idara ya mahakama nchini Kenya, AJS imekuwa njia muhimu ya kushughulikia mrundikano wa kesi Mahakamani. Zaidi ya maswali halisi ya nambari na ufanisi, AJS ni mbinu ya kifalsafa ya kina yenye athari kubwa katika elimu ya sheria na mahusiano ya binadamu.

Mnamo tarehe 4 Machi 2016, Jopokazi la Mifumo Mbadala ya Haki liliteuliwa kuangalia *Mifumo mbalimbali ya Kitamaduni, Isiyo Rasmi na Mingineyo Inayotumika Kupata Haki Nchini Kenya (Mifumo Mbadala ya Haki)*. Lengo kuu la Jopokazi lilikuwa kuchunguza mfumo wa kisheria, kisera na kitaasisi wa AJS ili kutekeleza mamlaka ya kikatiba ya Mahakama kwenye Ibara ya 159(2)(c) ambayo inaitaka Mahakama kuendeleza njia mbadala za utatuzi wa mizozo ikiwemo mifumo ya kitamaduni ya utatuzi wa mizozo. Lengo la Jopokazi lilikuwa kubuni sera ya kukuza ushirikiano thabiti na maelewano kati ya Mifumo Mbadala ya Haki na mfumo wa Mahakama, pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki na utoaji wa haki kwa haraka. Malengo haya yamejumuishwa kwenye mkakati wa hivi majuzi zaidi wa mahakama uliofafanuliwa katika *Mwongozo wa Mabadiliko ya Mahakama Endelevu.*

1.2 Mchakato wa Kuunda Sera

Sera hii ilitengenezwa kupitia mfululizo wa midahalo na mafunzo. Wakati jopokazi lilikusanya na kulinganisha nyenzo ambazo zimetumika kutengeneza waraka huo, hatua ya kwanza ilikuwa na sifa ya kujifunza kwa pamoja kwa wanajopokazi, watumiaji wa AJS na viongozi wa mbinu za AJS. Mawazo mengi yamejaribiwa na kutolewa maelezo muhimu katika desturi za AJS kwenye desturi za kitamaduni, pamoja na vyanzo vinavyohusishwa na mawazo ya kila siku ya haki. Maelezo ya kina zaidi ya mazungumzo haya yamenaswa kwenye waraka wa Sera ya Msingi ambayo ndiyo msingi wa sera hii ya Mfumo. Mazungumzo ya jopokazi na wahusika wa AJS yalijikita katika kuelewa, kueleza na kujadili mbinu mbalimbali za kushughulikia aina nyingi za dhuluma zinazohitaji kuangaziwa. Jopokazi liligundua eneo hili kuwa eneo lenye nguvu na gumu lililojaa mbinu shindani, dhana tofauti za haki na viwango tofauti vya utendaji. Kama vile mchakato wa kuunda sera haukuwa msingi wa jopokazi, sera imependekeza mchakato wa utekelezaji ambao ni wa mabadiliko na unaoongozwa na washikadau wote.

1.3 Mtazamo wa Kihistoria

Kabla ya uvamizi wa kikoloni, jamii nchini Kenya zilikuwa na mifumo yao ya haki. Ukoloni, hata hivyo, uliweka mifumo miwili ya haki. Mfumo mmoja, Mahakama za Wenyeji, ulitumia sheria za kimila kwa jamii za kiasili (ambazo zilijulikana kama 'Wenyeji') na ulishughulikia sheria za familia, umiliki wa ardhi, na masuala ya urithi. Mfumo wa pili, Mahakama za Jimbo la Kikoloni, ulitumia sheria iliyopitishwa kutoka Uingereza na mifumo mingine ya kikoloni kwa walowezi. Ingawa Serikali kuu ya kikoloni ilikusudia kuunganisha mifumo hiyo miwili ya kisheria, iliwekea mipaka matumizi ya sheria ya kimila kupitia 'kifungu cha mkinzano, ambacho kilisema kuwa sheria ya kimila ingetumika mradi tu haikinzani na haki na maadili. Haki na maadili, mwishowe, vilitafsiriwa kutoka kwa mtazamo wa Sheria ya Kawaida ya Uingereza na Waingereza.

Mwishoni mwa utawala wa kikoloni, Katiba ya Kenya ya 1963 ilitambua mifumo ya kitamaduni ya utatuzi wa mizozo kama sehemu ya mfumo wa sheria wa baada ya ukoloni wa Kenya. Mifumo ya kitamaduni ya mizozo, hata hivyo, ilitumika tu kwa kiwango ambacho haikuwa 'inakinzana na sheria yoyote iliyoandikwa'. Sheria ya Kimila ya Kiafrika iliwekwa kwenye safu ya chini kabisa ya ngazi ya kisheria: chini ya Katiba, Sheria za Kenya, Sheria za Waingereza za Matumizi ya Jumla, na Sheria ya Kawaida. Hata hivyo, kwa sababu Waafrika walitumia mifumo rasmi na isiyo rasmi, kuliendelea kuwa na mwingiliano mkubwa kati yao na haikuwa busara kutarajia mifumo hiyo miwili kufanya kazi ikiwa tofauti. Ilikuwa ni lazima ifanye kazi kwa pamoja na iliathiriana katika suala la mchakato na matokeo.

Katiba ya 2010 ilifufua nafasi kuu ya Sheria ya Kimila ya Afrika na mifumo ya kitamaduni kupitia Ibara ya 159(2)(c) ambayo inaipa Mahakama mamlaka ya kuendeleza mbinu za kitamaduni za utatuzi wa mizozo na wakati huohuo kuziweka mbinu hizi chini ya mfumo wa haki za binadamu wa Sheria ya Haki [Ibara ya 153(3)]. Kwa hivyo, matumizi ya "kitamaduni", "kimila" au "mbadala" ("Mifumo Mbadala ya Haki ") imeendelea kudumu.

2.0 Mantiki na Muktadha

2.1. Mazingira Yaliyopo

Historia ya Kenya inategemea njia nyingi za kupata haki. Kuna mizozo mingi inayotokea katika maisha ya kila siku, lakini ni michache sana kati ya hiyo ambayo hutatuliwa na Mahakama rasmi. Badala yake, nyingi kati yao inatatuliwa kwa kutumia Mifumo Mbadala ya Haki (AJS). AJS ndiyo maana ya kina ya kile ambacho Katiba inarejelea katika Ibara ya 159(2)(c) kama mifumo ya kitamaduni, isiyo rasmi na mingineyo inayotumiwa kupata haki nchini Kenya. Licha ya mamlaka ya kikatiba, AJS bado haijafanywa kuwa taasisi na hakuna miongozo ya kutosha ya kisheria na kisera ya kusimamia AJS. Kwa hivyo jopokazi liliazimia kuchunguza jukumu la AJS katika msururu wa haki na kutoa mwongozo wa jinsi ya kuhakikisha kuwa mbinu za AJS zinasimamiwa kwenye maelezo ya Katiba.

Katika utafiti wao, Jopokazi liligundua kuwa AJS ni sehemu ya maisha ya kila siku ya Wakenya na inafaa katika kuongeza upatikanaji wa haki kwa watu. Mnamo 2007, utafiti wa Sekta ya Utawala, Haki, Sheria na Utaratibu (GJLOS) uligundua kuwa imani katika Mahakama iliendelea kuwa ndogo. Utafiti wa baadaye wa Idara ya Mahakama, pamoja na Taasisi ya Hague ya Ubunifu wa Sheria uligundua kuwa ni asilimia 10 pekee ya Wakenya wanaotumia mfumo rasmi wa haki kutatua mizozo yao (Tazama Utafiti wa Mahitaji ya Haki na Kuridhika Nchini Kenya, 2017). Uchunguzi wa majaribio uliofanywa na Jopokazi unaonyesha maadili muhimu ya kijamii na kitamaduni yanayozunguka AJS nchini Kenya. Kando na desturi za kila siku za AJS, ni dhahiri kwamba jamii zilizofanyiwa utafiti zimefanya jitihada za kulinda, kuhifadhi na kukuza tamaduni zao. Tafiti za nyanjani pia zilithibitisha kuwa AJS ni mbinu ambayo Wakenya kote nchini, katika maeneo ya mashambani na mijini, huiomba wanapokuwa na mizozo. Hii inatokana na faida nyingi zinazotolewa na mikutano hii, ikilinganishwa na Mahakama rasmi. Ukweli kwamba mifano hiyo imetolewa kutoka kote nchini inathibitisha kwamba mbinu hii ya utatuzi wa mizozo imeenea.

2.2. Masharti ya Kujihusisha na AJS

2.2.1 Matakwa ya Katiba

Katiba ya Kenya inaweka wajibu kwa idara ya mahakama Kukuza Mfumo Mbadala wa Haki. Pia inathibitisha maono ya kuchochea na kupanua uhuru wa raia kutumia wakala wao, kujiendesha kwa uwajibikaji na kuwafanya walio na mamlaka wawajibike kwa matendo yao. Masharti haya yamefafanuliwa kwa kina katika vifungu vingi vinavyohimiza upatikanaji wa haki kwa wote, hasa Ibara ya 10, 48, 50, 159 na 174. (Angalia Kiambatisho p. x)

2.2.2 Mifumo ya Kikanda na Kimataifa

Kenya imetia saini mikataba kadhaa ya kimataifa na kikanda ya haki za binadamu ambayo inakuza upatikanaji wa haki kwa wote. Hizi ni pamoja na Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu.

(UDHR); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR); Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake (CEDAW); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICESCR); Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Binadamu na Haki za Watu (Mkataba wa Banjul); Itifaki ya Mkataba wa Kiafrika wa Binadamu na Haki za Watu wa Haki Kuhusu Haki za Wanawake Barani Afrika (Itifaki ya Maputo); Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC). Katiba ya Kenya ya 2010 inaweka wazi kwamba sio tu kanuni za jumla za sheria za kimataifa zinachangia sehemu ya sheria za Kenya bali pia mkataba au makubaliano yoyote yaliyoidhinishwa na Kenya.[1]

2.2.3 Umuhimu wa AJS

(a) AJS inaonyesha hali halisi ya maisha ya Wakenya na ni mchakato mwafaka wa kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wakenya wengi.

(b) AJS kama mfumo wa kupanua haki za binadamu na uhuru wa binadamu: AJS ni chombo muhimu cha kupanua haki za binadamu. Kwa sababu AJS ni uhalisia unaoishi, inabadilika na kuendana na hali mpya na ina uwezo wa kushughulikia mabadiliko ya kisheria na kwa hivyo inaendana na kanuni za haki za binadamu.

(c) AJS kama mbinu ya kutenda haki kwa njia tofauti na kwa ufanisi zaidi: AJS inatimiza hili kwa angalau njia sita - (i) haina uhasama na ni aina ya haki ya kurejesha; (ii) inahakikisha ushiriki zaidi wa kijamii kwa kuwa ni shirikishi zaidi; (iii) ni nafuu zaidi; (iv) ina urasmi na ufundi mdogo na inazingatia haki thabiti; (v) ni ya haraka zaidi; na (vi) haina uhasama na inajumuisha suluhu nyingi za kiubunifu.

(d) AJS ni mbinu mwafaka ya kupunguza mrundikano wa kesi na kupunguza msongamano wa Mahakama: Mojawapo ya masuala makuu ya mfumo rasmi wa haki nchini Kenya ni mrundikano mkubwa wa kesi. Kwa hiyo, kupunguza mrundikano katika Mahakama ni mojawapo ya malengo ya msingi ya Mahakama. Kwa kushughulika mizozo ifaayo na kuzuia kwa bidii mizozo mingine kuongezeka, AJS inapunguza msongamano wa kesi Mahakamani.

(e) AJS ni mbinu ya kuingiliana upya kijamii na (na kuhalalisha tena) Nchi: Mojawapo ya malengo ya mabadiliko ya Katiba ni kuhalalisha tena Nchi kwa kuleta Serikali karibu na wananchi. Mifumo Mbadala ya Haki huongeza ushiriki wa umma katika mfumo wa haki na hivyo kuwashirikisha tena watu na Serikali.

(f) AJS ni mbinu ya kuunda upya Serikali na Raia kama sehemu ya mradi wa kikatiba wa kuunda upya Serikali ya Kenya: AJS inalenga kuimarisha jukumu la Serikali na Raia kama wahusika wa moja kwa moja wanaochangia katika uhuru wao wa kiraia. Mamlaka nyingi za taasisi za AJS hazitokani na mamlaka zilizokabidhiwa Serikali na watu wa Kenya, badala yake, zimetoka moja kwa moja kwa wananchi. Kwa hivyo, AJS inalenga kuimarisha jukumu la Serikali na raia kama wahusika wa moja kwa moja wanaochangua katika uhuru wao wa kiraia.

(g) AJS ni njia ya kudai upya kanuni za kitamaduni na kama mradi wa kurejesha zile za kitamaduni kama za kimantiki: Mbinu ya AJS huhifadhi na kukuza tamaduni na kuzizuia kuwa "chakavu" na kwa hivyo inafaa katika maisha ya kisasa.

1 Tazama Ibara ya 2 (5) & (6).

2.2.4 Changamoto kwa Utekelezaji wa AJS

Ingawa mbinu za AJS zinatumiwa na Wakenya wengi wanaotafuta haki, na kutekeleza jukumu la ziada kwa mifumo rasmi ya haki, zinakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo:

Ukosefu wa kutambuliwa: Katiba ya Kenya ya 2010 inatambua utatuzi mbadala wa mizozo na kuinua hadhi yake hadi kanuni ya mahakama. Hata hivyo, AJS haijatambuliwa rasmi kama tawi linalosaidiana katika utoaji wa haki.

Ukosefu wa haki za kijinsia: Mbinu za AJS mara nyingi zinatawaliwa na wanaume na zinaonekana kutoa nafasi ndogo kwa wanawake kama wafanya maamuzi. Zaidi ya hayo, kwa sababu vikao vingi vya AJS ni vya wanaume, mizozo inayoathiri wanawake au wasichana inachukuliwa kuwa haiwezi kushughulikiwa kwa njia ya haki na nyeti.

Watu Waliotengwa na Walio katika Mazingira Magumu: Mbinu za AJS zinaonekana kuwatenga makundi yaliyotengwa na watu walio katika mazingira magumu.

Ukosefu wa uwajibikaji na Kudunisha Katiba: AJS haidhibitiwi na kwa hivyo haina mbinu mwafaka za uwajibikaji. AJS inaonekana kukosa haki ya kiutaratibu pamoja na kudunisha maadili na majukumu ya kikatiba, k.m. jukumu la Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP). Pia, kuna wasiwasi kwamba baadhi ya matokeo ya Mbinu za AJS huenda yasipatane na viwango vya kikatiba na haki za binadamu.

Sera hii inazingatia kwamba mbinu za AJS, kama vile michakato yote ya utatuzi wa mizozo, zina changamoto fulani huku ikitambua kwamba uhuru wa kufuata utamaduni na dini ya mtu ni haki ya kimsingi ya binadamu. Sera hiyo na Miongozo huruhusu uundaji wa mbinu na tafsiri mbadala ambazo zitafungua nafasi ya changamoto kwa imani za kitamaduni. Sera hiyo inaweka njia ya kutambua na kusisimua Mbinu za AJS huku ikipunguza changamoto zilizobainishwa kupitia mfumo thabiti wa haki za binadamu unaohusisha ushirikishwaji wa kina wa Mbinu za AJS pamoja na kupitishwa kwa mafundisho yanayofaa ya kubainisha ufikiaji wa mamlaka wa Mbinu za AJS pia kama mafundisho ya uendeshaji juu ya mwingiliano kati ya Mbinu za AJS na Mahakama.

2.2.5 Uchanganuzi wa Uwezo, Udhaifu, Nafasi, Matishio (SWOT)

Licha ya changamoto zinazoikabili AJS, mbinu hiyo pia ina uwezo na fursa zake ambazo zimefupishwa hapa chini katika uchanganuzi wa SWOT.

Uwezo	Udhaifu
• Mahitaji na Matumizi ya juu ya AJS • Ufahamu wa AJS • Kesi za AJS zinazoendeshwa kwa lugha ya wenyeji na zinatumia utamaduni wa wenyeji unaoeleweka na watu • Inahusisha ushirikishwaji na ushiriki wa jamii • Kuzingatia na kutumia haki ya urejeshaji • AJS haina uhasama na inatoa suluhu bunifu • AJS ni nafuu • AJS ina mamlaka juu ya masuala ya kiraia na kihalifu	• Ukosefu wa mfumo wa kisheria na sera • Ukosefu wa ufadhili uliowekwa kwa AJS • Mtazamo wa AJS kuwabagua wanawake, watoto na watu waliotengwa • Ukosefu wa Uwajibikaji • Ukosefu wa mchakato wa uteuzi/ uchaguzi kwa wazee na wahusika wa AJS • Ukosefu wa Mamlaka iliyoainishwa kwa AJS • Ukosefu wa Mbinu za Utekelezaji • Baadhi ya tamaduni ni changamoto kwa viwango vya jumla vya haki za binadamu • Wanawake, vijana na walemavu kutengwa kwa mchakato wa kufanya uamuzi • Ukosefu wa nyaraka za mchakato na maamuzi
Nafasi	**Matishio**
• Katiba ya Kenya ya 2010 • Mifumo ya Kisheria ya Kikanda na Kimataifa • Uratibu kati ya AJS na mfumo rasmi wa mahakama	• Ukosefu wa maarifa na ujumuishaji wa mfumo wa haki za binadamu na wahusika wa AJS • Ukosefu wa uwezo na mafunzo kwa wahusika wa AJS • Kufahamiana na wanaozozana kunaweza kusababisha ufisadi au upendeleo kwa watoa maamuzi • Vikao vya AJS vinaweza kufanywa kuwa vya kisiasa na kubadilishwa • Ukosefu wa majukumu yaliyobainishwa kwa Utawala wa Kitaifa, Mambo ya Ndani na Kaunti

3.0 Mipango ya Sera ya AJS

3.1. Mfumo wa Haki za Binadamu na Mbinu za AJS

Ibara ya 159(2)(c) inawajibisha Mahakama kuendeleza AJS. Hii ina maana kwamba mfumo wa AJS uliopitishwa nchini Kenya utalazimika kuingiliana na Mahakama na kwa hivyo muundo wa haki za binadamu - usawa ufaao kati ya uhuru wa raia na maadili ya kikatiba ni muhimu. AJS inapanua haki za binadamu kwa sababu mbinu zake zimeegemezwa kwenye njia tatu zenye msingi wa haki za binadamu: Ibara ya 48 ambayo inaamuru Serikali kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote; Ibara ya 10 na 28 ambayo inaeleza maadili ya kitaifa na haki ya heshima; na Ibara ya 44 ambayo inasisitiza haki ya kila mtu kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni anayochagua. Mfumo huu wa haki za binadamu sio tu wa kifalsafa, pia unaonyesha mazingatio ya vitendo ya AJS.

3.1.1 **Wajibu wa Kuheshimu** unahitaji kutoingiliwa na Serikali katika kufurahia haki na uhuru. Hili linahitaji Mahakama na vyombo vingine vya Serikali kuhakikisha kwamba hakuna kuingiliwa kwa mchakato wa AJS kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hata hivyo, wajibu huu haukosi vikwazo - pale ambapo kuna madai ya ukiukaji wa haki za binadamu kwenye mchakato wa AJS, Mahakama na vyombo vingine vya Serikali lazima vichunguze mchakato wa AJS, lakini lazima vifanye hivyo kwa namna ambayo inaambatana na Katiba.

3.1.2 **Wajibu wa Kulinda** – Hili linahitaji kuundwa kwa sheria, sera na kanuni za AJS ambazo zinalinda dhidi ya ukiukaji wa haki za binadamu na kutoa suluhu kwa ukiukaji huu. Kwenye nguzo hii, Idara ya Mahakama ina wajibu wa kisheria kuchunguza mazingira ya ukiukaji wote au madai ya ukiukaji wa haki zinazolindwa katika Ibara ya 159.

3.1.3 **Wajibu wa Kubadilisha** – Katiba ya Kenya ni Katiba ya mabadiliko ambayo ina maana kwamba inahakikisha kuwa Serikali inatimiza wajibu wake kwa kuleta mabadiliko makubwa. Lengo la Katiba ni kuanzisha mabadiliko na mageuzi ya kijamii kwa kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijamii uliokuwepo nchini Kenya. Hii ina maana kuwa vikwazo vya usawa wa kijamii vinapaswa kuondolewa na badala yake kuwekwa mfumo unaowezesha haki ya kijamii. Kwa hivyo, Mahakama haina budi kuhakikisha kwamba tabia ya mabadiliko ya Katiba inadumishwa katika michakato yote ya AJS wakati wote. Kuhusiana na: Taasisi huru za AJS - Mahakama lazima iweke viwango vya chini zaidi kwa wahusika wa Serikali ili kuhakikisha kuwa wanafuata maadili ya kikatiba; Wahusika wa Tatu - Mahakama inatakiwa kurekebisha mapungufu yaliyopo katika vyombo vinavyotekeleza AJS na mchakato wa AJS wenyewe; na AJS Iliyounganishwa na Mahakama - Idara ya Mahakama inahitajika kuunda na kutekeleza, kwa nia njema, Mpango wa Utekelezaji wa michakato na mbinu za AJS.

3.2. Miundo ya Mifumo Mbadala ya Haki na mapendekezo ya sera

Jopokazi lilitambua njia tofauti ambazo AJS inatekelezwa na kuziweka katika aina nne kuu (aina): Taasisi huru za AJS, Taasisi Huru za AJS za Wahusika wa Tatu,

Taasisi za AJS Zilizounganishwa na Mahakama na Taasisi za AJS Zinazodhibitiwa na kupitisha tatu za kwanza. Ifuatayo ni maelezo ya kila moja:

3.2.1. **Taasisi Huru za AJS:** Hii ni mifumo huru ambayo inaendeshwa na jamii. Jamii inaamua wafanya maamuzi na michakato inayopaswa kufuatwa bila kuingiliwa kati au kudhibitiwa na Serikali. Wafanya maamuzi waliochaguliwa wanatatua mizozo hii kwa kutumia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza jamii husika.

